COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD

Wednesday, 22nd November, 2023

Third Assembly – Second Session
NINTY SIXTH SITTING

[The County Assembly met at 10:36a.m at the County Assembly Buildings]
[The Temporary Speaker (Honourable Abdirahman Abdikadir) in the Chair]

PRAYERS

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Please take your seats. I do understand that there are some Members in the Committee room; can you alert them to come in before we proceed with this Sitting. Honourable Allen Katana, please just go ahead and usher in other Members...

[Hon. Allen Katana whipped the Honourable Members]
[Silence]

Yes Clerk?

MOTION

ESTABLISHMENT OF WATER TRANSPORT INFRASTRUCTURE FOR ENHANCED AND MOBILITY AND ECONOMIC GROWTH

Yes, Honourable Allen Rodgers Katana, MCA Shanzu Ward please move the Motion.

Hon. Katana: Thank you, Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, I beg to move the following Motion;

AWARE THAT Mombasa County, being encompassed by the vast expanse of the Indian Ocean, holds a unique geographical advantage that can be optimally utilized to foster water transport;

FURTHER AWARE THAT the implementation of water transport, facilitated by ferries and boats has the potential to substantially augment revenue streams, invigorate tourism and enhance overall transportation efficiency within the County;

UNDERSCORING the exemplary models witnessed in Lamu, where speed boats efficiently ferry passengers and goods between the mainland and islands, as well...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Order Honourable Katana! I can see you are straining your eyes put on your glasses please!

Hon. Katana: Let me put on my glasses...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** ...Or are we on the same subscription!

[Interruption]

Hon. Katana: I am not so sure.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Is it in order to propose another Member to read for you?

Hon. Katana: No, I will manage; with your due respect and permission, I can use my step mother's Honourable Baimu's glass!

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Please take it!

Hon. Katana: Thank you; you are the best Speaker on planet earth! Thank you, Mr. Speaker, the exemplary models witnessed in Lamu, where speed boats efficiently ferry passengers and goods between the mainland and islands, as well as in Dar es Salaam and Zanzibar in Tanzania, Istanbul in Turkey and Dubai in the United Arab Emirates (UAE). These models have not only proven successful but have significantly contributed to economic growth and increased mobility;

NOTING THAT the establishment of a comprehensive water transport system in Mombasa County aligns with the successful practices observed in similar coastal regions globally, presenting a viable opportunity for economic development;

RECOGNIZING THAT the implementation of water transport infrastructure has the potential to create employment opportunities and entrepreneurial ventures for the youth and residents of the County;

Mr. Speaker,

ASSERTING THAT water transport not only facilitates efficient mobility but also serves as a sustainable and environmentally friendly alternative, alleviating congestion on existing road networks;

CONCERNED THAT the untapped potential of Mombasa's Coastal advantage for water transport might impede the County's ability to fully capitalize on economic opportunities and tourism potential;

Mr. Speaker Sir,

SERIOUSLY CONCERNED THAT the absence of a comprehensive water transport system may hinder the County's ability to meet the evolving transportation needs of its residents and businesses;

Mr. Speaker,

I, therefore, urge this August Assembly to RESOLVE:

1. *THAT the County government expeditiously…*

   Mr. Speaker let me repeat this *THAT the County government expeditiously initiates a thorough feasibility study to assess the viability of establishing water transport infrastructure, drawing inspiration from successful models in Lamu, Dar es Salaam, Zanzibar, Istanbul and Dubai;*

2. *THAT the County government collaborates with relevant maritime authorities, private investors and international experts to develop and implement a strategic plan for the establishment of a robust water transport system, encompassing ferry and boat services;*

3. *THAT public awareness campaigns be promptly launched to educate residents on the myriad benefits of water transport, garnering community support for the initiative.*

Now, Mr. Speaker allow me to kindly ask Honourable Juma Manuari to second this very important Motion.

Hon. Juma Manuari: Mr. Speaker Sir, I second.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Honourable Manuari, next time you wait for the Speaker to give you the chance.

Hon. Juma Manuari: Okay Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdulkadir)**:** Okay. Yes, Honourable Allen Katana you may take off your glasses now and then make your contribution.

Hon. Katana: Ahsante Mheshimiwa Spika umeanza kusema nitoe miwani, haya labda umeona hayajanipendeza lakini naona yako sawa na nguo niliovaa lakini kwa mwelekeo huo tutaenda hivyo. Kwanza nitoe shukrani Mheshimiwa Spika ya kupata nafasi hii tena; nichukue nafasi hii kukupongeza Mheshimiwa Mwenza wa Old Town kwa sababu katika zile timu za Waheshimiwa ambao ni wageni katika Bunge hili Mheshimiwa Spika timu yake Mheshimiwa huyo wa Old Town ndio iliyo wahi kwenda mpaka kiwango ilichofikia.

Mheshimiwa Spika wacha inakiliwe katika kumbukumbu za Bunge hili ya kwamba katika timu zote zile zilizokuwa zimebaki katika kile kipute hichi cha Mheshimiwa Spika mimi ilikuwa naunga mkono timu ya Mheshimiwa Abdirahman ambayo kwa kweli hiyo ndio timu ambayo ilikuwa imebaki ya katika Waheshimiwa wapya wa Bunge hili...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Honourable Katana…

[Interruption]

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, usisikie vibaya ilikuwa naendelea...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Honourable Katana, am still recovering from yesterday's defeat and your sentiments are not doing me any favour! Please let us stick to the agenda of this Motion, however thank you very much for your support. Proceed.

Hon. Katana: Ahsante Mheshimiwa Spika, hata ilikuwa nimebana wasijue ni wewe lakini kwa kuwa umejitambulisha pole. Mheshimiwa Spika, nikirudi kwa suala la leo ni kwamba wacha inakiliwe katika kumbukumbu za Bunge hili ya kwamba serikali hii na Bunge letu limetumia fedha ya kuwapeleka hata Waheshimiwa ili hata kwenda kujifunza hata katika nchi zengine. Mheshimiwa kilichotuma nilete Hoja hii Bungeni na niombe Waheshimiwa hawa wakaweze kupitisha kwamba usafiri umekuwa donda sugu tukizingatia kwamba jimbo letu la Mombasa limezingirwa na mzunguko wa maji. Kwa hivyo nikawaza na vitu ambavyo niliviona katika sehemu nilizo ziorodhesha ikiwemo Zanzibari kule Tanzania, Turkey, Dubai ile miundo misingi iliyowekwa, wakatumia viombo kama nivyo orodhesha hapa ambavyo vimeurahisisha sana usafiri katika sehemu zao. Mheshimiwa Spika, kunazo sehemu ambazo zikifunguliwa itakuwa hatutegemei tu magari kuingia katika jiji letu na kwenda sehemu zengine za mji wetu wa Mombasa. Ndio nikaona hoja hii Mheshimiwa Spika nilete Bunge ili Waheshimiwa, nikitilia maanani ya kwamba kila Mheshimiwa aliye hapa ana nakala yake na ameipitia. Hivyo basi niwaombe Waheshimiwa Wenza wakaweze kuiunga mkono hoja hii, ili tukaweza kupitisha na tuishughulikie…

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Order! Order! Honourable Mbaya and Honourable Juma Mwalimu, is there anything you would like to share with us? I can see you are consulting loudly. Yes, Honourable Mbaya?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii ambayo ilikuwa sijaiomba, isipokuwa sina la kuongezea kwa sasa ahsante Mheshimiwa Spika…

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Okay Honourable Juma? Do you have anything to say?

Hon. Juma Mwalimu: Ndio Mheshimiwa Spika, nilikuwa namwambia Mheshimiwa Mbaya kwamba hii hoja lazima tuichangie kwa sababu, ina maana sana kwetu sisi ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Okay, next you will do it on the floor thank you, so proceed please Honourable Allen.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika kwa kuwa nimesoma hali ilivyo humu Bungeni na Waheshimiwa wameelewa Mswada huu, kwa heshima yako ukianza na Mheshimiwa Juma aliyesimama tu mda mfupi ulioisha kwa sababu, sitaki kukuelekeza ingekuwa ni vizuri tuunge mkono Mswada huu mara moja, ili tukaweze kwenda nyumbani tuangalie mambo mengine. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Thank you. Yes, Minority Leader? Or is it Leader of Minority? Please proceed.

The Leader of Minority (Hon. Matsaki)**:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Mimi pia wacha nisimame kama Mheshimiwa aliyechaguliwa na pia namshukuru Mheshimiwa mwenza kwa kuleta hoja hii. Kwa kweli ukiangalia hali ya usafiri hasa kwenye hii miji, tukisema angazia hilo jambo hapa Kaunti ya Mombasa, ni jambo ambalo limeleta shida sana. Hata tunaposema kwamba barabara zizidi kupanuliwa kisha bado sioni kwamba kutakuwa na mabadiliko. Kwa hivyo ni hoja nzuri hasa Mheshimiwa Allen Katana allivyoleta hapa Bunge, ni vyema sisi pia Waheshimiwa tuweza kukubali na kuipitisha kwa sababu, zaidi ya yeyote ikiwa labda ni Kaunti itaweza kununua vyombo kama hivi, pia itakuwa inaongeza riba ama ushuru kwa Kaunti yetu. Pili itapunguza pia msongamano wa barabarani kwa sababu unapokuwa unataka kuja jiji mapema basi inakubidi wewe uondoke saa kumi na mbili ikiwa wewe ni mkaaji wa Kisauni na saa tatu ukitoka saa hizo basi itakuwa ni shida. Kwa hivyo mimi naunga mkono hoja hii, wacha tuipatie kipao mbele na heshima kwa Waheshimiwa wenza watamuunga mkono pia Mheshimiwa Allen Katana ahsanteni sana.

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Thank you Leader of Majority… Yes? Honourable, pardon Leader of Minority! Yes, Honourable Juma Mwalimu?

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante Mheshimiwa Spika. Nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii kuweza kuchangia Mswada huu ulioletwa na ndugu yangu Mheshimiwa Allen Katana.

[Applause]

Kama ilivyo kawaida yangu, mimi ni wale miongoni wa kuunga mkono kila Mswada hapa, sijajizoesha kupinga…

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Pardon, say that again please?

Hon. Juma Mwalimu: Hujasikia Mheshimiwa Spika?

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Yes, say that again.

Hon. Juma Mwalimu: Nasema kama kawaida yangu, mimi ni wale miongoni wa kuunga mkono Miswada apa Bungeni sijajizoesha kupinga na pia...

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Honourable Juma Mwalimu, are you saying you will support any Motion that comes before the House; whether it is good or bad for the people of Shika Adabu of Mombasa?

Hon. Juma Mwalimu: Potelea mbali Mheshimiwa Spika!

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Okay.

Hon. Juma Mwalimu: Mimi naunga Mswada.

The Temporary Speaker (Hon. Abdulkadir Abdirahman)**:** Have you withdrawn that statement or you are going to stick to that?

Hon. Juma Mwalimu: Ipi hiyo?

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** That you are going to support every Motion?

Hon. Juma Mwalimu: Naunga tu.

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** All the Motions?

Hon. Juma Mwalimu: Pengine nijifundishe saa hizi kupinga…

[Laughter]
[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Okay Honourable Juma Mwalimu you are within your rights to support or object any Motion please, proceed.

[Laughter]

Hon. Juma Mwalimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi naunga mkono Mswada huu kwa sababu, ukipingwa au ukipitishwa na kutekelezwa itakuwa ni faida sana kwetu sisi watu wa Likoni kwa sababu, huu usafiri wa miundo msingi ya wasafiri wa kwenye maji kama sisi tunaovuka pale Ferry utakuwa umetusaidia sana kwa sababu ukiangalia hali ya saa hizi kule Likoni kila kukicha mitaa inazidi kufurika watu wa kutoka sehemu mbali mbali kuja kupata nyumba kule. Saa hizi watu wa Majengo, wa Mvita wote wamekimbilia Likoni kwa hivyo kumekuwa kuna msongamano mkubwa pale Ferry, hata saa hizi Ferry zinazosafirisha watu ni tano lakini hazitoshi. Kwa hivyo kukiwekwa miundo msingi bora pengine kuletwe boti za kiserikali ama za Kaunti, itakuwa umeturahisishia sisi kwa usafiri juu kama tulivyoona miezi kadha iliyopita, tulikuwa na *floating bridge* na ilikuwa hali ya kuvuka ilikuwa rahisi.

Lakini kwa sasa ile *floating bridge* hakuna na kumezidi kuwa na msongamano wa magari na watu, sasa Ferry hazitoshi. Kwa hivyo tukiweka huu muundo msingi ambao ndugu yangu Mheshimiwa Katana alikaa na akafikiria, sisi itakuwa ametufaidi zaidi. Kwa hivyo kwa maana hii ndio nizidi kusisitiza ya kwamba nitaunga mkono Mswada wowote ule ambao uko na maana na manufaa kwa watu wa Mombasa na Shika Adabu kwa jumla. Ahsante sana Mheshimiwa Spika na pia vile vile nitasema hongera kwa mchezo wa jana ingawa, kuna kushinda na kushindwa ahsante...

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdikadir Abdirahman)**:** Thank you. Yes, Honourable Nusura?

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nataka nimpe pongezi sana Bwana Allen Katana kwa kuleta hoja hii ndani ya Bunge hili. Mimi kwanza nataka niseme kwamba natoka Mtongwe mimi na tumeathirika sana sana kwa mambo ya Feri, ahsante sana Bwana Allen kwa kunikumbusha...

[Applause]

Mimi kama kiongozi wa Mtongwe ambaye ni Mwakilishi Wadi wa pale, kama nisingesimama kuchangia hoja hii nitakua nimechaguliwa bure na wale watu wangu wa Mtongwe. Shida tunazo zipata watu wa Mtongwe kwa sababu ya Ferry, nafikiri ni miaka isiopungua labda ishirini na tano kufikia sasa kwa sababu, ni tangu 1994 Ferry kuzama, tumeanza kupata shida ya usafiri pale sisi, japokuwa mara inaletwa inafanya masaa matatu, inafanya masaa manne saa nyengine, lakini hayatoshi wakaazi wa pale ni wengi na shida zilizokuweko pale ni nyingi. Kwa sasa hivi wale ambao wako na mijengo ndani ya Mtongwe wameathirika sana wamepata hasara sana na majumba yao majumba hayana wapangaji lakini hoja hii imeletwa wakati mzuri. Pia ningependa kuiomba serikali ya Kaunti, Mheshimiwa Spika na kupitia Waheshimiwa wenza ndani ya Bunge hili kuipitisha hoja hii endapo itapita na natumai itapita kwa sababu sisi sote hapa ni waathiriwa; aidha wa barabara ama wa usafiri wa ndani ya maji. Kwa hivyo ningeomba pia serikali yetu ya Kaunti iweze kuangalia swala hili kwa sababu ni mambo madogo ambayo yamebakia pale; tulijengewa mteremko pale watu wakawa wamekuwa na matumaini ya kupata feri pale shida ni ndogo sana. Huu upande wa pili, huku kulikuwa kunatafutwa nafasi ili kujengwe mteremko pia kule watu wa Mtongwe nao waweze kupata usafiri wa feri pale ili waweze kupata faida pia ya matunda ya ugatuzi wa Kaunti. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika nimesimama kuiuunga mkono sana, sana, sana. Ahsante Bwana Allen. Ahsante Bwana Spika.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Thank you Honourable Nusura. There are two gentlemen who are up; okay, yes Honourable Frankline?

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika na mimi nasimama pia kuunga mkono hoja hii na kabla niweze kuendelea uturuhusu ama uniruhusu Mheshimiwa Spika nimpongeze Mheshimiwa wa Mji wa Kale ambae kwa sasa labda hajafika katika Bunge hili.

Lakini sisi kama wawakilishi Wadi tunajivunia kwa weledi wake, ujuzi wake wa yeye kuwa mkufunzi mkuu na pia kuwa mfadhili mkuu wa timu ile ambayo inatoka Mji wa Kale. Vijana wale walionyesha ujuzi wa kusakata kabumbu na sisi tunampongeza na tunamuombea Mungu aiponye roho yake kwa haraka kwa yale yaliyompata. Mheshimiwa Spika tukirudi kwa hoja ya leo, Mheshimiwa nasimama kuunga mkono tukizingatia ya kwamba Katiba yetu ya Kenya katika Ratiba ya 4, sehemu ya 2 ya Katiba ya Kenya, 2010 imepeana mamlaka na najaribu kuitafuta hapa Katiba yangu Mheshimiwa Spika labda ukinipa nusu sekunde, nimeipata: *The Fourth Schedule of the Constitution part 2 that is the functions of the County government* Bwana Spika, *one of the functions of the County government is County transport which includes:*

a) County roads;
b) Street lighting;
c) Traffic and parking;
d) Public road transport; and
e) Ferries and harbours, excluding the regulation of international and national shipping and matters related thereto.

Therefore, the issues of ferries and harbours Mr. Speaker, ferries and harbours is a County function…

[Applause]

Na kile cha kushangaza Mheshimiwa Spika na labda mimi ningemuomba Mwakilishi Wadi wa Shanzu almaarufu *Hodikoo* ni kwamba hata zile feri kwa sasa zimewekwa katika halmashauri ya Bandari (Kenya Ports Authority) ambalo ni shirika la serikali kuu, zile feri zinafaa kuwa chini ya uongozi wa serikali ya Kaunti. Mheshimiwa Spika, inamaanisha ya kwamba endapo Mswada huu utapita, na baada ya kupita Kamati husika ya Utekelezaji iweze kuwajibika na Waziri wa Usafiri na Miundo Misingi pia aweze kuwajibika, kuna uwezo wa kubadilisha mji wetu wa Mombasa kufika viwango ambavyo kwa kimombo wanasema 'International Standards'. Mheshimiwa Spika, kwa hivyo mimi ninaposimama kuunga mkono hoja hii siuungi tu mkono kwa sababu imeletwa na rafiki yangu lakini nauunga mkono kwa sababu iko na misingi ya kisheria imeuungwa mkono na Katiba ya Kenya na hivyo inamaanisha hata wale mabwana ambao saa hii wametoka serikali kuu wamekuja nasikia wanapigapiga kelele hapa Mombasa kupayuka payuka kutukana uongozi wa Mombasa waambiwe kwamba pia sisi sheria twazijua na yanayostahili kufanya na serikali ya Mombasa twayajua na yanayofaa pia kufanywa na hao wanafaa wafanye bila kuja kutupigia kelele. Mji wa Mombasa una wenyewe na wenyewe ndio sisi hapa ambao tunafanya maamuzi kama Gatuzi, ahsante Mheshimiwa Spika.

[Consultations]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Honourable Juma…

[Interruption]

Hon. Makanga: Na kama ni noma, iwe noma…

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** No! No! No!

[Laughter]

I do not think that is a parliamentary statement to make Hon. Frankline Makanga. It is not Parliamentary to make such statements you are not in a rally here to whip emotions. Yes, Member of the Speaker's Panel, a fellow Member please make your contribution.

Hon. Hamisi Nyota: Ahsante Mheshimiwa Spika. Leo nataka nichangie hoja hii kwa lugha ya Kiswahili…

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** So, is that something unusual?

Hon. Hamisi Nyota: Hapana, kwa sababu mimi nishazoea mara nyingi huongea lugha ya kimombo, kwa ueledi wangu wa lugha ya kimombo ndio huwa mara nyingi kwenye Bunge hili Mheshimiwa Spika husimama na kuchangia hoja nyingi kwa lugha ya kimombo lakini leo nimeamua nirudi nyumbani nichangie hoja hii kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Kwanza kabisa Mheshimiwa Spika nataka kuchukua fursa hii kumpongeza ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Allen Katana Mheshimiwa wa kule Shanzu. Mheshimiwa Spika kwa kweli mji wetu wa Mombasa kama alivyotathmini kwenye huu Mswada wake ni kuwa sisi tumekalia katika sehemu nzuri ya kufaidika na uwepo wa bahari Hindi ambayo tuko nayo hapa Mombasa. Kwa kuwa tukiweka misingi muhimu ya kisheria na tukiweka mikakati mizuri hii misongamano tunayopata katika barabara zetu na katika miji yetu vijijini kuja mjini, itakuwa ni swala la kuwa ni la urahisi na ni swala ambalo litakuwa limetusongeza mbele kama mji mkubwa wa pili hapa katika nchi yetu ya Kenya.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ni kweli Mheshimiwa Allen Katana nampongeza kwa kuwa hoja hii alivyoiunda, alivyoileta kweli ikipita hoja hii basi itakuwa imepunguza kwa kiasi kikubwa misongamano tunayoiyona barabarani hususan pale mvua ndogo inaponyesha, kwa sababu nasema hili jimbo letu la Mombasa ni mji ambao umezungukwa na bahari hivyo basi kukiwekwa mikakati mizuri ya kuleta usafiri kutoka Mombasa bara (Mainland) kuja kisiwani itakuwa ni jambo lingine zuri Mheshimiwa Spika kwa sababu itarahisisha usafirishaji wa bidhaa, itarahisisha usafirishaji wa watu na hii misongamano ambayo tunaishuhudia kwa sasa hivi. Kwa muda huu, barabara zetu ni ndogo na idadi ya watu Mombasa inazidi kukuwa kila uchao, kwa hivyo itakuwa ni muhimu Bunge hili na wenzangu kuwasihi pia, tusimame pamoja tupitishe hoja hii kwa sababu manufaa yake ni makubwa kuliko vile alivyoelezea Mheshimiwa Allen Katana. Haya manufaa yanayopatikana katika hoja hii Mheshimiwa Spika ni makubwa zaidi na yataleta natija na kufanya Mombasa uwe mji ambao umepiga hatua mbele Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo mimi nasimama kidete niukiunga mkono asilimia mia kwenye huu Mswada, shukran sana Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Thank you Honourable Nyota for your contribution. Your command of Swahili language is brilliant as well, so I recommend you be contributing in Kiswahili language going forward. Yes, Honourable Mbelle from Bamburi who has witnessed some floods in his area and knows a thing or two about water transport. Please contribute.

Hon. Mbelle: Thank you, Mr. Speaker Sir and I do not want to say that you were wrong while you say he should contribute in Kiswahili but I feel like you might have faulted his ability and eloquence in English, so kindly continue advising him to contribute in Kiswahili and also in English as much as he can. Mr. Speaker Sir, I am proud of my *shemeji* which is a Swahili word; *shemeji* in English I think English have faulted a little bit, brother- in-law for bringing such a matter. Sorry my Deputy Chair here is telling me is called *Mkazamwana* which is the wrong word. Mr. Speaker Sir, water transport for me is one of the means and ways of how our County can in so many ways be able to uplift the economic standards of this city, particularly when it comes to reducing the turn-around time in matter of business administration and even implementation. When you are to take cargo from Mombasa to Shanzu let us say Shanzu via road and probably via sea, it will take less time on sea and it would impact more lives particularly on people that would be loading and offloading and it would be cheaper and it is not just about cargo but even people being transported. Mr. Speaker Sir, I also want to note that in our current Annual Development Plan (ADP) I have just read that there is supposed to be a feasibility study that should to be done in the year 2024/2025 by the department of Transport and Infrastructure which is going to cost Kshs 15 million but that feasibility study is earmarked on transport planning management and safety. So, I am hopeful that we will implement it as it is, put in the ADP of course we have not passed the ADP yet but with the Motion and with the discussion we are having right now I think is one of the reasons why I will support the passing of ADP when it comes to this House.

[Applause]

Again Mr. Speaker Sir, I also see that in the same budget in this current financial year 2023/2024 there is another feasibility study that is supposed to be carried out on the construction of jetties and infrastructure around water transport, which was supposed to cost the County up to Kshs 6 million. The feasibility study is supposed to be carried out this financial year; we are not yet done with the financial year, so am hopeful that the transport and infrastructure department would actually carry the feasibility study which will also guide us in the next financial year as we are looking at implementation on the rest. Mr. Speaker Sir, I also note in the Annual Development Plan that in the year 2024/2025 and in the subsequent year of 2025/2026 there has been set Kshs 25Million in 2024/2025 for the construction of a jetties for water transport and in the year 2025/2026 there is two more jetties are supposed to be constructed at a tune of 45 Million Shillings. So, I feel and hope that even during the Governors manifesto as he read his manifesto and when he was giving his maiden speech, he actually talked about putting a lot of effort in water transport and I have already felt it in the ADP.

All that am hopping is that we will actually do what is in the ADP as per the interest of this House because everybody will be standing up to talk about this matter, they all be in support knowing that very well is going to bring in lots of fortune to the people of Mombasa. Mr. Speaker Sir, I also want to recognize that even in the Blue Economy department as much as we do not have money for construction of jetties and feasibility studies in such matters, it is also important to say that as the Chairperson and probably as the Members of the Blue Economy Committee do fully support this Motion knowing very well that is going to uplift the blue economy standards of this particular County. So, thank you Mr. Speaker Sir and I fully support this Motion and again wish to congratulate my brother-in-law from Shanzu Mr. Allen Katana, Honourable on this particular matter and also wish to congratulate yourself and Honourable Nyundo for the exemplary and wonderful match that you had yesterday.

Sorry, that the Honourable Member lost from Old Town; but again, his team has always been a team to reckon with when it comes to matters of football. So, thank you Mr. Speaker Sir, and again I support this Motion. Thank you.

The Temporary Speaker: (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Thank you Honourable Mbele. Yes, Honourable Sylveter Kai from Junda Ward.

Hon. Kai: Thank you.

The Temporary Speaker: (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Are you going to do your contribution in English or in Kiswahili?

Hon. Kai: Ahsante, nafikiri ni Kiswahili.

[Applause]

The Temporary Speaker: (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Please proceed.

Hon. Kai: Shukran. Nitakuomba ruhusa siku nyengine niweze kutoa mapendekezo yangu kwa lugha ya mama kama utaniruhusu; kwanza niseme, nichukue fursa hii kupeana furaha zangu kwamba ile timu ambayo ilikuwa nasapoti jana iliweza kushinda ambayo niya ndugu yangu Nyundo.

The Temporary Speaker: (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Let us stick to this subject matter.

Hon. Kai: Kisha nikirudi kwa mada yetu ya leo**,** unajua mimi na ndugu yangu Samir Bhaloo tumeweza kupakana tu labda kwa kilomita chache, labda mbili hivi lakini tumegawanywa na mkono wa bahari ndio maana unaona majina yetu yakafanana Tudor na Junda kwa sababu nikama tu sehemu moja na sote ni UDA. Ahsante, hivyo basi hii hoja ambayo ameweza kuleta ndugu yangu Allen Katana naona ni nzuri sana na ikiweza kupitishwa itaweza kuleta wepesi sana na mimi kama mkaazi wa Junda nahisi itaweza kunifaa sana, lakini pia nasimama kuunga mkono lakini akikubwa zaidi nilikuwa nimesimama ilinipeane furaha zangu kwa ushindi ulotokea jana. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker: (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Honourable Sylvester Kai, you are taking it personal now. Honourable, I do not know now, who is senior? Are you the senior between the two of you?

Hon. Salim Mbaya: I am the senior.

The Temporary Speaker: (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** You are the senior. Yes, Honourable Manuari please take your seat! Honourable Mbaya, please make your contribution, I am made to understand that he wants to make his contribution via sign language, are there Members of the House who understand sign language? Okay, please let us take turn our attention to the sign language interpreter.

[Hon. Salim Mbaya signing]

Hon. Salim Mbaya: Thank you, Mr. Speaker. I stand to support this Motion…

[Applause]

Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Honourable Mbaya, you have used so many minutes just to say thank you Mr. Speaker. However, I commend you for your effort in learning the sign language and I say to you…

[Interruption]

Honourable Mbelle, point of information!

Hon. Mbelle: Mr. Speaker Sir, I wish to inform the House that in as much as we support this Motion, again it is important to note that even in our vocational training institutions we have not put a lot of emphasis when it comes to matters of water transport. Probably, it is important that as we are supporting at some point, we add the aspect of making sure that we have people who are trained because in this day and time we buy those sports or even those jetties there is a high possibility that not most of our youth will be the ones constructing or being capacitated to actually drive or operate those locomotives. So that was my information.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Well, noted but that sounded more of a contribution than point of information. But nonetheless it has been accepted. Yes? It is for the Speaker to rule that Honourable Kai, any other Member wishing to make a contribution? Yes, Honourable Mwaura.

Hon. Mwaura: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niungane na wenzangu kuzungumzia Mswada huu ambao umeletwa na ndugu yangu Mheshimiwa Allan Katana. Niseme kwamba ninauunga mkono Mswada huu ni kwamba kama jinsi Mheshimiwa Kai alivyozungumza mimi nimekuwa kwa mda mara kwa mara nikitembea maeneo yake na ninaona watu wengi wakitoka sehemu hiyo na wanavuka mjini kupitia barabara. Ingekuwa iko rahisi kabisa kama hii ingekuwa imetekelezwa; wavuka tu Tudor na waingie mjini na kwa vibarua bila kutumia njia ndefu na kutumia fedha nyingi za kukuja kupitia kwa barabara. Mheshimiwa Spika, hofu yangu kubwa ni moja peke yake, kupitia kwa huu Mswada kwamba unahitaji pesa nyingi tu kutengeza bajeti kununua hizo vifaa vya ubaharini. Tunaelewa sio vitu ama sio vifaa ambayo viko bei rahisi na hii ndio iingie katika bajeti yetu tunahitaji kuipitisha na pia kufuatilia tuone kama miaka ijayo tutaziweka katika bajeti ila nimesikia mmoja akisema hakikishe imetekelezwa kwa haraka. Utekelezaji wa huu Mswada mimi nataka kusema ya kwamba sitaki kuzungumza kwa niaba ya Kaunti lakini fedha zinazohitajika katika kutekeleza huu Mswada ni fedha nyingi. Na….

[Interruption]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Pengine kwa mtazamo wako ni fedha kiasi gani?

Hon. Mwaura: Siwezi kusema labda Mwenyekiti anayehusika kwa mambo ya baharini anaweza kutuambia lakini naweza kukadiria ni fedha nyingi zinazohitajika. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika ni kueleza tu ya kwamba tuipitishe huu Mswada alafu pia tuangalie maana hili Bunge ndio linaolipitisha hii bajeti na bajeti ijayo tupitishe tukizingatia maswala hayo. Naunga mkono Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Ahsante Mwenyekiti.

[Interruption]

You have a point of information? Okay please inform us.

Hon. Mbelle: Mr. Speaker Sir, I wish to get permission from my fellow learned Member because he knows a lot about agriculture and Kongowea so, he is learned on all those matters. I just wish to inform him that in the County flagship projects as captured in the Annual Development Programme (ADP) it says that the County government will collaborate with national government for the PPP that is Public Private Partnerships the relevant development partners and provide legal frameworks for water transport to be effective and that has been given timeline of 2023/2027 which is supposed to be implemented by the Directorate of Water transport and infrastructure and MIC. So, I think as he says in as much as it is expensive but there is already a framework that has been given in the county flagship projects which might be able to guide him further. Thank you, Mr. Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** I want to believe the Chairperson Committee on Implementation has been informed reliably. Let us proceed. Yes, Honourable are you standing or scouting?

Hon. Juma Manuari: Ahsante Mheshimiwa Spika. Unajua mimi nimesimama nikiangalia aliesimama maana najua nikisimama na mwenzangu mimi nitakaa tu; wengine ni *senior* kuniliko. Mheshimiwa Spika, kwanza nikupe pongezi kwa ule mchakato wako uliofanya jana Mungu akuwezeshe. Kwa sababu katika timu yako kuna wajomba zangu na vijana wangu ambao walicheza vizuri pale kwa hivyo mwaka ujao tuna hakika Mungu akipenda ile kitu tutachukua tu. Mheshimiwa Spika, mimi nisimame niunge ndugu yangu Rodgers mkono kwa huo mchakato aliouleta na vilevile tangia mapema nilivyotaka kusimama kuongea ilikuwa ni swala ambalo ndugu yangu Mbelle ameligusia kuwa shughuli yoyote ya bahari ni kwa ushirikiano wa watu watatu. Hawa ni serikali kuu, serikali ya Kaunti na wale wanarubuni ambao wako kule nyanjani ambao wanataka kubadilisha miji yetu, kwa mfano kina World Bank na wale wengine wengine kwa kuwekeza pesa zao katika hili swala la maendeleo.

Tunajua kweli ni hoja nzuri tumeileta lakini tumeileta hoja hii ni jukumu letu kama Kamati itakuwa inahusika na maswala kama haya turudini tena kwa Gavana tumketisheni chini tumpe mwelekeo kama huo yeye kama kiongozi ili hili swala akilibeba na yeye aombe ridha kutoka kwa serikali kuu na wale wahusika ambao watakuwa wako kule ili tuje tukaeni meza moja ya mzunguko tuone jinsi gani tutakizungumzia swala hili. Kwa sababu nitakupa mfano ulio hai; kuna wakati mmoja ferry za Likoni zilikwama walikuwa na mgomo kwa siku moja tu lakini ilikuwa na shida siku hiyo mpaka dunia nzima ikazungumza kwa sababu ile ferry ya Likoni ni sawa sawa na muunganisho wa jamii ya Africa mashariki (East African Community) gari zote mwelekeo wote hupita na pale.

Kwa hivyo huo wakati ferry zilivyogoma sisi kama Mabaharia wa eneo wa Likoni tulitumia madau yetu kuvukisha watu ng'ambo ya pili lakini baadae Port Police na serikali kuu ilibidi walete askari tuondolewe baharini. Kwanza, tukaambiwa kiusalama hatuna *safety gears* kimombo wanavyosema tukatolewa baharini na tukaambiwa pia hatuna kithibitisho ama leseni ya kutufanyisha sisi kuvukisha watu katika maeneo yale. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika Mswada wa ndugu yangu ni mzuri ila tukitoka tu hapa na ile Kamati husika kwa sababu hapa kuna Kamati ya Uchukuzi na Kamati ya Maji ambazo tutakuwa tuko pamoja na Kamati ya utendaji kazi.

Hizi ni Kamati lazima ziwe zitakuwa zinashirikiana kwa pamoja turudini kwa Gavana tumpeni muelekeo huu tumuambie sisi kama Wabunge tumekuja na hoja hii na imeletwa na ndugu yetu Katana na sote tukakubaliana nayo na wewe uipime na wale viongozi wengine walioko kule ili wakikaa pamoja kwa sababu muungano wa serikali hizi mbili ndio yule mwekaji nini atakuja na tutafanya shughuli yetu iwe itakuwa inafana. Hivyo basi Mheshimiwa Spika tusiwe tu wengi wa kusema na tukitoka hapa twayaacha kwenye vipakatilishi yaje yasikizwe siku nyengine siku nyengine baada ya miaka mitatu ije irudishwe hoja hino hino na baada miaka mitatu irudishwe hoja hino hino jambo kufanyika halifanyiki lakini sisi yetu ni kusema tu kwa sababu mdomo nyumba ya maneno na kazi yetu tuliyotumwa hapa sio ya kukoroga sege ni ya kusema. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika mimi naliunga swala hili mkono. Ahsante.

[Applause]

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Thank you Honourable Manuari. Any other Member wishing to make his or her contribution?

[Silence]

Okay, Honourable Katana as you respond please make sure you address the issues or contributions raised by most of the Members; as the issues of ferries which has been raised which was not part of your Motion try to see how you can contribute to that so please take your time and contribute to the Motion effectively.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumza chenye kimetajwa na chenye ambacho kiko katika hoja yetu ya leo. Kwanza niwashukuru Waheshimiwa hawa kwa hoja walizozileta na nikizingatia kwanza maudhui hasa ya hoja hii kwanza ni kuhakikisha sisi wenyewe tulio hapa nikitoa mfano wa mimi mwenyewe Mheshimiwa Spika nimepigiwa kura ama nimeajiriwa hapa na watu 4500 lakini na wengi tuliwaahidi vitu vingi ya kwamba tutawapa makazi lakini makazi hakuna. Sasa katika suluhu ya ni vipi tutatafuta kazi ndio nikawaza kuja na Mswada huu ilhali endapo hivi vidau vitapatikana kupitia serikali ya Kaunti ama watu binafsi cha msingi Mheshimiwa Spika ni miundo msingi iwekwe ili watakapoingilia na watakapofikishwa iwe kuna urahisi wa kushuka na kuabiri.

Hivyo basi, hususan nikitoa mfano Dubai kuna watu wanaingia tu na wanavuka ng'ambo ya pili, si kwa kusudi wanashughuli wanaenda kufanya lakini wanafurahia kuabiri ndani ya bahari pale pale mbali na utalii Mheshimiwa Spika kuna vijana ambao wanaendesha vidau vile na hawakosi riziki za kupeleka kwao majumbani. Mheshimiwa Spika, swala lengine ambalo linaweza ama lilinituma Mswada huu kuuleta Bungeni Kaunti yetu ya Mombasa si sawa sawa na Kaunti kama Rift valley, si sawa sawa na Kaunti za Kilifi na kwenda huko mbele. Nasema hivyo kwa sababu gani Mheshimiwa Spika na si kwamba nazidhalilisha Kaunti zengine lakini ni kwa sababu kimombo wanasema Mombasa Kaunti ni *City County*!

Hatuna pesa nyingi ambazo twaweza ekezea mashinani eti zimekwenda kwa sababu ya kwenda kununua mbolea watu walime mashamba ili Mombasa Kaunti Mheshimiwa Spika ionekane baadhi ya Kaunti ambazo zimeleta maendeleo na zimeleta mapato makubwa ni lazima iwekeze katika mambo kama haya ya usafiri wa kupitia baharini. Mheshimiwa Kai aliposimama ameongea kuhusu Junda na Tudor; ziko sehemu tu nyingi leo hii Mheshimiwa Spika nikija mimi sikutaka kukuambia nimekupigia nikakudanganya kwamba niko Bunge lakini nilikuwa sijafika niko barabarani kwa sababu nimeshikwa na msongamano mkubwa wa magari nikatamani. Mheshimiwa Spika, pangekuwa na usafiri wa baharini ambapo nikifika ni kidau naingia Pirates na nashuka hapa kwako Old Town. Mheshimiwa Spika, kuna sehemu nyengine kama ya kisiwa hiki kuunganisha na kwa Mheshimiwa Nusura kama alivyosema Mheshimiwa Spika, kuna sehemu nyingi ambazo kwa hakika endapo swala hili Waheshimiwa wako hapa kama Mheshimiwa wa Kongowea Mheshimiwa Mwaura anasema itaigharimu serikali hii pesa nyingi, pesa nyingi ni za kwako?

[Laughter]

Mheshimiwa Spika, tuko hapa kwa ajenda mbili; ajenda ya kwanza, ni kuhakikisha kwa mbinu yoyote tunatafuta maisha ya watu wetu yawe nirahisi kuyaishi, pili kwa kuwa tumeajiriwa na wananchi na tukawaahidi tutawapa kazi hatuna njia zengine hata njia zengine ni kama hizi. Mheshimiwa Spika, utakuta tukiwa na hawa vijana wetu watapata ajira na zaidi ya kupata Mheshimiwa Spika nitakupa mfano kidau nilichoingia mimi ni kisiwa cha Dubai kwenda upande mwengine wa mji wa kale wa Dubai imetengezwa na Mbao! Mbao! Na kivuli chake ni tonobari, hata Kiti ulichokalia kimetengezwa na tonobari. Sasa huu ughali mimi siwaoni Mheshimiwa Spika endapo tutapata tunaweza anza kuwe na vidau ishirini hapa vidau ishirini pale, vidau ishirini pale! Tukianzia hapo Mheshimiwa Spika tutakuwa tumeleta ajira kwa watu wetu na tutakuwa tumerahisisha usafiri katika katikati ya jiji na zaidi ya kurahisisha usafiri katikati ya jiji tutakuwa tumeongeza utalii, kama nilivyokuambia sikuwa na biashara ng'ambo nyengine lakini nilivuka tu kufurahia mahandhari. Mheshimiwa Spika, nisiongee kuzidi hapo niwaombe Waheshimiwa wenzangu ili Mswada huu tuupitishe na tutakapo upitisha kupitia kwa Mheshimiwa wa Kongowea ambaye ndiye Mwenyekiti husika wa kusukuma haya maneno tushirikiane nae kwa sababu hata hiyo bajeti inapotajwa ADP na sijui vitu gani vyengine haviwezi kufanya kazi mpaka sisi tunachokijua kinamfaa mwananchi wetu ni sisi na ile serikali na ile *executive* itafuata ule ushauri ambao sisi tutapeana hapa. Kwa hayo machache nisiongee kupitiliza, niwaombe Waheshimiwa wenza kwa sauti ya kunyenyekea, kwa sauti moja tupitishe swala hili. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Temporary Speaker (Hon. Abdirahman Abdikadir)**:** Brilliant! Thank you, Honourable Katana for your response to the Motion and I want to believe that most Members have internalized your message today. Honourable Members, I now put the question that the Motion by Honourable Allen Katana on Establishment of water transport infrastructure for enhance mobility and economic growth be adopted in this Honourable House in the same term as moved.

[Question put and agreed to]

The Motion by Honourable Allen Katana on Establishment of water transport infrastructure for enhanced mobility and economic growth is adopted in this Honourable House. Yes Clerk?

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Wednesday 22nd November, 2023 at 2:30p.m. Thank you.

The House rose at 11:38a.m.